

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 □ DAR ES SALAAM □ TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA TANZIA



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, anasikitika kutangaza kifo cha **Dkt. Novetha Kigombe** (1980-2021), kilichotokea tarehe 26 Oktoba 2021 katika Hospitali ya Mlonganzila.

Marehemu **Dkt. Kigombe** alikuwa Mhadhiri katika Idara ya Sanaa Bunifu, Ndaki ya Insia. Alianza kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mkufunzi Msaidizi mwaka 2006 na kupanda vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Mhadhiri mnamo mwaka 2014, cheo alichokuwa nacho hadi alipofariki.

Dkt. Kigombe alikuwa msomi na mwanataaluma aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika maeneo ya Utawala katika Sanaa za Maonesho.

Mipango ya mazishi inafanywa na familia ya marehemu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ibada na itifaki ya kumuaga itafanyika Alhamisi tarehe 28 Oktoba 2021 saa saba mchana nyumbani kwake, Kibamba, Dar es Salaam, na kisha kusafirishwa kwenda katika kijiji cha Mpepai, Wilaya ya Mbanga, Mkoa wa Ruvuma kwa mazishi.

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!

Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano kwa Umma
27 Oktoba 2021